# JIMBO LA IRINGA

## HOSPITALI YA TOSAMAGANGA

*Barua zote ziandikwe kwa:*
*Mkurugenzi Mkuu wa Hopitali*
*Barua pepe.tosamagangacdh1970@gmail.*

S.L.P11,
TOSAMAGANGA,

Kumb.Na.Doira.Vol.063/10 22.03.2023

# TANGAZO LA KAZI

Mkurugenzi Mkuu wa Hospitali ya Tosamaganga iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, kufuatia kibali chenye **kumb. Na.Fa.10/128/01 'M"/77** cha tarehe **27.02.2023** kutoka kwa **Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala bora**, anawatangazia nafasi za kazi watanzania wote wenye sifa ili kujaza nafasi kama zilivyo orodheshwa katika tangazo hili.

**1. AFISA MUUGUZI MSAIDIZI DARAJA LA II (ASSISTANT NURSING OFFICER II) NAFASI - 1**

**SIFA ZA MWOMBAJI**

Kuajiriwa mwenye elimu ya kidato cha nne au cha sita na mwenye stashahada (**Diploma**) ya Uuguzi na kutoka vyuo vinavyotambulika na Serikali na awe amesajiliwa na Baraza la Wauguzi na Wakunga Tanzania (**Tanzania Nusrsing and Midwife Council**).

**MAJUKU YA KAZI**

I. Kufanya kazi za kiuguzi na ukunga, kuhudumia wateja katika jamii, Hospitali na sehemu zote zinapotolewa huduma za afya
II. Kukusanya takwimu muhimu za afya
III. Kutoa huduma za wagonjwa majumbani
IV. Kutoa huduma za kinga na uzazi
V. Kutoa ushauri nasaha
VI. Kufanya kazi nyinigine atakazopangiwa na kiongozi wake wa kazi

**MSHAHARA**

Mshahara utalipwa kwa kuzingatia ngazi ya serikali wa na **TGHS B**

THE DIRECTOR GENERAL
P.O.Box 11
TOSAMAGANGA
TOSAMAGANGA HOSPITAL

CamScanner

## 1. AFISA MUUGUZI II (NURSING OFFICER II) – NAFASI - 1

### SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa mwenye elimu ya kidato cha nne au cha sita na mwenye Shahada (**Degree**) ya Uuguzi na kutoka vyuo vinavyotambulika na serikali na awe amesajiliwa na baraza la wauguzi na wakunga tanzania (**Tanzania Nusrsing and Midwife Council**).

### MAJUKUMU YA KAZI

I. Kufanya kazi za kiuguzi za kuhudumia wateja katika jamii, Hospitali na sehemu zote zinapotolewa huduma za Afya.
II. Kukusanya takwimu muhimu za Afya.
III. Kuwaelekeza na kusimamia wauguzi walio chini yake.
IV. Kutoa huduma kwa wagonjwa majumbani.
V. Kutoa ushauri nasaha.
VI. Kutayarisha mpango wa kazi kwa ajili ya huduma za uuguzi.
VII. Kutoa huduma za kinga na uzazi
VIII. Kuelimisha wagonjwa na jamii
IX. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake

### MSHAHARA

Mshahara utalipwa kwa kuzingatia ngazi ya serikali wa na **TGHS C**

### MASHARTI YA UJUMLA KWA WAOMBAJI WA NAFASI ZOTE

1. Waombaji wote wawe raia wa tanzania
2. Waombaji wote wawe na umri wa kuanzia miaka **18** na usiozidi miaka **45**
3. Waombaji wote waambatanishe nakala za vyeti vya elimu na taalima kwa mujibu wa sifa ya kada
4. Waombaji wote waambatanishe nakala ya kitambulisho cha **NIDA**
5. Waombaji waambatanishe **"CV"** zao zenye anuani na nambari za wadhamini wasiopungua wawili
6. Maombi yatumwe kwa yatumwe kupitia anuani ifuatayo

Mkurugenzi Mkuu,
Hospitali ya Tosamaganga,
S.L.P 11,
**Tosamaganga - Iringa.**

**N:B** Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **04.04.2023** saa Tisa na nusu **(9:30)** Alasiri

PB

THE DIRECTOR GENERAL
P.O.Box 11
TOSAMAGANGA
TOSAMAGANGA

CamScanner

Paolo Belardi

..............................

**PAOLO BELARDI**

**KNY: MKURUGENZI MKUU**

THE DIRECTOR GENERAL
P.O.Box 11
TOSAMAGANGA
TOSAMAGANGA HOSPITAL

**Nakala kwa :-**

- Mkurugenzi Mtendaji,
  Halmashauri ya Wilaya ya Iringa,
  S.L.P 108,
  Iringa – Tanzania.